

Abdul Hassan Mshaweji  
Mstaahiki Meya Manispaa  
Songea

# Songea yetu

JARIDA LA MANISPAA YA SONGEA



TOLEA NAMBA MBILI

APRILI-JUNI 2019



M/S Tina Sekambo  
Mkurugenzi Manispaa  
Songea

## Tatizo la maji Manispaa ya Songea kubakia historia

TATIZO la maji katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma litabakia kuwa historia baada ya serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt John Magufuli kutoa kiasi cha zaidi ya Dola milioni 50 kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa maji katika kata zote 21 na mitaa yote 95 iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea. Akizungumza katika Mkutano wa Baraza la madiwani la manispaa ya Songea, Mbunge wa Jimbo la Songea mjini na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki Dkt. Damas Ndumbaro amesema mradi huo unatekelezwa na nchi ya India na kwamba mradi una-

tarajia kuanza Septemba 2019. Hata hivyo amesema hali ya upatikanaji wa huduma ya maji pembezoni mwa mji wa Songea ni asilimia 46.6

### Kituo cha Afya Ruvuma kuhudumia wakazi 45,000

MRADI wa ujenzi wa kituo cha afya Kata ya Ruvuma unatarajia kutoa huduma kwa wakazi zaidi ya 45,000 wanaoishi katika kata za Ruvuma, Subira, Mateka na majengo.

Mhandisi wa Ujenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea Mhandisi Karoline Bernad amesema ujenzi umekamilika ambapo hadi sasa majengo yote manne yakiwemo maabara, upasuaji, wagonjwa wa nje na mama na mtoto yamekamilika.



Mbunge wa Songea Mjini  
Dkt. Damas Ndumbaro

## YALIYOMO

- TATIZO LA MAJI KUBAKIA HISTORIA
- TASAF YABADILISHA MAISHA YA KAYA MASIKINI
- BARAZA LA MADIWANI LAPITISHA BAJETI YA BILIONI 41
- SERIKALI YATOA MILIONI 100 KUJENGA MADARASA
- HIFADHI YA ASILI YA LUHIRA ILIYOPO SONGEA
- IFAHAMU MANISPAA YA SONGEA
- MAPATO STENDI YA M FARANYAKI YAONGEZEKA KWA ASILIMIA 300

## TASAF ilivyobadilisha maisha Songea

MPANGO wa kunusuru kaya maskini kupitia TASAF awamu ya III, katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea ulianza kutekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea kuanzia kipindi cha mwaka wa fedha cha 2015/2016, jumla ya mitaa 53 imenufaika na mpango na idadi ya kaya zilizofikiwa ni 4,878.

Mratibu wa TASAF katika Halmashauri hiyo Christopher Ngonyani amesema katika kipindi cha Julai hadi Januari 2018/2019 Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs.530, 75,780.00** Kwa ajili ya kuwalipa walengwa **4,878** sawa na asilimia 100 ya walengwa wote kwa lengo la kusaidia kaya masikini kujikimu kiuchumi.

Baadhi ya wanufaika wa TASAF katika Manispaa hiyo wameelezea namna walivyobadilisha maisha yao, akiwemo Demotiana Milanzi (48) Mkazi wa Makambi ambaye ameweza kununua uwanja na kujenga nyumba ya bati ya vyumba vinne katika eneo la Mshangano, Mnufaika mwingine ni Halima Komba (46) mkazi wa Mjimwema ambaye ameweza kununua bati 32 na kufanikiwa kuezeka nyumba yake ambayo kwa miaka mingi aliezeka kwa turubai na kuishi kwa tabu.

**Madiwani wa Manispaa ya Songea wakiwa kazini Manispaa ya Songea**



## Sekondari 4 Songea zapewa mil.100

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma Tina Sekambo amekiambia kikao cha Baraza la madiwani wa Halmashauri hiyo kuwa serikali imetoa shilingi milioni 100 katika shule 4 za sekondari ili kutekeleza mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa. Shule hizo ni sekondari ya Mataka, Msamala, Lizaboni na Matarawe.

**Mradi wa maji Luhirakati wakamilika**  
Mradi wa maji Luhirakati Kata ya Mwingemshindo Manispaa ya Songea, unaonufaisha watu 941, umegharimu sh. milioni 490 umekamilika. Vituo 16 vya kuchotea maji vimejengwa



**Mti unaoongoza kwa ugumu duniani uliogundulika Manispaa ya Songea**

MTI unaoaminika kuwa unaoongoza kwa ugumu na kuishi miaka mingi duniani umegundulika katika Makumbusho ya Taifa ya Majimaji mjini Songea

Mhifadhi Kiongozi wa Makumbusho ya Taifa Majimaji Mhifadhi Kiongozi Barthazar Nyamusya anautaja mti huo kuwa unafahamika kwa jina la Chikunguti ambao ulitumika kama alama kwenye kaburi la shujaa wa vita ya Majimaji Nduna Songea Mbano ambaye aliuawa na kuzikwa mwaka 1906 mti huo ukiwa upo.

Inakadiriwa mti huo hivi sasa utakuwa na miaka zaidi ya 125. Kulingana na Mhifadhi huyo aina hiyo ya miti ina uwezo wa kuishi hadi miaka 1000.

**Mndeme aagiza Manispaa ya Songea kukusanya mapato kwa zaidi ya asilimia 80**



MKUU wa Mkoa wa Ruvuma Christina Mndeme akiwa na Kamati ya ulinzi na usalama Mkoa na wilaya ya Songea aliongoza kikao maalum kilichofanyika kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea, ambacho ajenda kuu ilikuwa ni Changamoto za ukusanyaji wa mapato katika Manispaa ya Songea, pamoja na mambo mengine Mndeme aliagiza Kuhakikisha katika mwaka huu wa fedha, Manispaa inakusanya mapato kwa zaidi ya asilimia 81. Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea Tina Sekambo amejipanga kuhakikisha kuwa mapato ya Halmashauri hiyo

yanapanda ili kufikia malengo ya liowekwa na serikali ya kila Halmashauri kukusanya mapato kwa zaidi ya asilimia 80. Sekambo hivi sasa amewapanga wakuu wa Idara na vitengo kuhakikisha wanasimamia vizuri mashine za kukusanyia mapato na kuongeza uhamasishaji wa matangazo ili kuhakikisha kila mfan-yabiashara na mtoa huduma anawajibika kulipa kodi kulingana na biashara anazofanya. Hadi kufikia Juni 2019 makusanyo yamefikia asilimia 90.



**Mkuu wa Wilaya ya Songea Polelet Mgema akikabidhi hundi ya sh. milioni 71 kwa vikundi 53 vya wajasirimali wadogo katika Manispaa ya Songea**

# Luhira hifadhi ya asili iliyopo mjini Songea



Hifadhi ya asili ya Luhira iliyopo mjini Songea ni moja ya kivutio adimu cha utalii kilichopo kilometa saba toka mjini Songea mkoani Ruvuma. Hii ndiyo hifadhi pekee ya asili katika nchi nzima iliyopo

mjini. Ina wanyama wa aina mbalimbali wakiwemo pundamilia, nyani, mbawala, kakakuona, aina 105 za uyoga, nyoka wa aina mbalimbali wakiwemo chatu na ndege wa aina mbalimbali. Hifadhi hii ilianzishwa mwaka 1973.

Hifadhi ya Luhira ina ukubwa wa hekta 600. Hifadhi hiyo ina wanyama wa aina mbalimbali wakiwemo pundamilia, pongo, fisimaji, nyani, tumbili, kakakuona, kobe na chatu. Tozo ya kiingilio kwa Raia wa Tanzania watu wazima

sh.2000, watoto wenye umri kati ya miaka sita hadi 16 sh.500 na Watoto chini ya miaka sita ni bure.

Sekta ya utalii katika Manispaa ya Songea imefungua milango ambapo hivi sasa vivutio vipya vya utalii vimeibuliwa na vya zamani vinatangazwa ili kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi. Miongoni mwa vivutio hivyo ni milima ya Matogoro, Makumbusho ya Taifa ya Majimaji na Luhira

**Hifadhi ya Luhira**  
ina ukubwa wa hekta 600. Licha ya hifadhi hiyo kuwa na wanyama wa aina mbalimbali wakiwemo pundamilia, pongo, fisimaji, nyani, tumbili, kakakuona,

## Mapato stendi ya Mfaranyaki yaongezeka kwa asilimia 300

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma Tina Sekambo amesema Halmashauri ya Manispaa hiyo imeanza kunufaika na mradi wa kituo cha mabasi cha Mfaranyaki ambapo ukusanyaji wa mapato umeongezeka kwa asilimia zaidi ya 300 na kwamba kodi ya vibanda pia imeongezeka toka kati ya shilingi 25,000 hadi

50,000 kwa mwezi hadi 250,000 hadi 300,000 kwa mwezi.

Sekambo amesema ongezeko hilo limetokana baada ya kufanyika ukarabati wa stendi hiyo ambao umefanywa na Benki ya Dunia kupitia miradi ya ULGSP kwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 550. Amesema wajasirimali wakubwa na wadogo wamevutiwa kufanya

biashara katika kituo hicho kutoakana na kuwa na mazingira



## Songea yapitisha bajeti ya zaidi ya bilioni 41



BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma limefanya kikao maalum cha kupitisha bajeti ya Halmashauri katika mwaka wa fedha wa 2019/2020 am-

bapo, kikao hicho kimepitisha bajeti ya zaidi ya shilingi bilioni 41.


Akizunguma katika Kikao hicho Mwenyekiti wa kikao ambaye pia ni Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea Alhaj Abdul Hassan Mshawaji amesema wamejipanga kusimamia ukusanyaji wa mapato na kwamba hawatasita kuchukulia hatua mtumishi yeyote wa umma ambaye atabainika kuhujumu mapato ya Halmashauri.

“Tutakuwa wakali kwa watumishi watakaobainika kutafuna mapato ya

Halmashauri, pia tumejipanga kuongeza vitega uchumi”, alisisitiza.

[Dira ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea ni kuwa kitovu cha uwekezaji na maendeleo ya viwanda ili kufikia maendeleo endelevu ya jamii 2025.](#)





Milima ya Matogoro

## Vivutio vya milima ya Matogoro

HAPA sio kilele cha Mlima Kilimanjaro bali ni kilele cha mlima Matogoro uliopo Manispaa ya Songea Mkoa wa Ruvuma wenye vivutio adimu vya utalii ambavyo bado havifahamiki na wengi. Mlima Matogoro ni chanzo mito mitatu ya Ruvuma, Luhira na Luegu. Kuna msitu mne na eneo zuri la kufanyia picnic pamoja na vivutio lukuki ambavyo havipatikani

**Songea ina ziada ya chakula tani 40,000**

HALI ya upatikanaji wa chakula katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma inaridhisha ambapo kuna jumla ya Hekta 24,340.8 ambazo zilimwa msimu wa 2016/2017 na kuzalisha tani 98,671.76. wakati mahitaji ya chakula ni tani 58,280 hivyo .

**Songea ina viwanda zaidi ya 500**

HALMASHAURI ya Manispaa Songea ina jumla ya viwanda 539 kati ya viwanda hivyo kiwanda kikubwa ni kimoja viwanda, viwanda vya kati 14, vidogo ni 158 na viwanda vidogo sana ni viwanda 371.

*“Kukamilika kwa mradi huu kutaofanya manispaa ya Songea kuwa na machinjio bora zaidi Tanzania”*

## Machinjio ya kisasa ya Songea yakamilika

UJENZI wa machinjio ya kisasa katika Kata ya Tanga Manispaa ya Songea umekamilika kwa asilimia 100. Mradi huu umetekelezwa kwa gharama ya zaidi ya bil.3.2 .Kukamilika kwa mradi huu kunafungua fursa mpya za uwekezaji na ajira.



## Bustani ya Manispaa inavyovutia wengi

UBORESHAJI wa bustani ya Manispaa ya Songea kupitia Mzabuni anayeendesha bustani hiyo, umeanza kuvutia wageni wanaotembelea mji wa Songea .Uchunguzi umebaini idadi kubwa ya wageni inakuwa kubwa siku za sikukuu na mwisho wa wiki.Hata hivyo Mzabuni anaendelea na kazi ya

uboreshaji ili kuhakikisha bustani hiyo inakuwa ya kuvutia na kubadilisha muonekano wa mji Songea.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhandisi Stella Manjanya amesema bustani imeujengea heshima mji wa Songea kwa kuwa wageni wengi wanaotembelea Mkoa wa

Ruvuma wamepata mahali sahihi pa kupumzikia na kuburudika kwa michezo mbalimbali na vyakula .

Mradi huu umefadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 399.



## Barabara za lami Songea zafikia asilimia 72

MRADI wa ujenzi wa barabara katika kiwango cha lami Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma umefikia asilimia 72 na unatarajia kukamilika Septemba 30,2019.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Tina Sekambo amesema Ujenzi wa barabara kiwango cha lami km 10.3 katika

barabara za kati kati ya Mji umeanza Machi 25, 2018 .

Anamtaja Mkandarasi aliyefuzu kujenga barabara hizo kuwa ni Kampuni ya SIETCO ya watu wa Jamhuri ya China na kwamba hadi kukamilika mradi huo utagharimu jumla ya Tshs. 10,960,078,230.00.

Barabara ta FFU Matogoro ujenzi wake umekamilika ambapo hivi sasa wananchi wananufaika.



*“Barabara ta FFU Matogoro ujenzi wake umekamilika ambapo hivi sasa wananchi wananufaika na barabara hiyo”.*

## Maambukizi ya VWU yapungua Songea

HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma imefanikiwa kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka asilimia **3.9** mwaka 2017 hadi asilimia **2.7** kufikia Disemba 2018.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Songea Dkt.Mameritha Basike amesema licha ya changamoto zinazoikabili sekta ya Afya katika Manispaa hiyo, elimu dhidi ya UKIMWI imesaidia kupun-

guza maambukizi ya UKIMWI.

Kulingana na Basike, huduma za Afya ya uzazi na mtoto zinatolewa katika vituo **29 na kwamba** Huduma zinazotolewa ni chanjo kwa Watoto chini ya mwaka mmoja, huduma kwa wajawazito na wazazi ili kuzuia maambukizi ya Ukimwi toka kwa Mama kwenda kwa Mtoto ikiwemo ushiriki wa akina Baba. Amesema vifo vya wajawazito vimeongezeka toka 188/100,000 mwaka 2006 hadi 202/100.000 mwaka 2018.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Christina Mindeme akimkabidhi laini ya simu ya TTCL Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Prof.Riziki Shemdoe katika uzinduzi wa kampeni ya watumishi wa umma kujiunga na TTCL kwenye ukumbi wa sekondari ya Songea Girls



Miongoni mwa watendaji wa mitaa na kata katika Manispaa ya Songea wakipewa mafunzo ya usimamizi wa fedha yaliyofadhiliwa na Benki ya Dunia .Jumla ya watendaji 116 wamepata mafunzo hayo ambayo yalifunguliwa na Mstahiki Meyya wa Manispaa hiyo Alhaj Abdul Hassan Mshaweji

**Rais Magufuli alivyozindua mradi wa umeme wa Grid ya Taifa Manispaa ya Songea**



Mradi wa bustani ya Manispaa ya Songea uliofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya sh.milioni 399. Bustani ipo jirani na Jengo la NSSF na Mkabala na Manispaa ya Songea. Mradi umeanza kazi na umeshaanza kuwanufaisha wakazi wa mji wa Songea.



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akiwa pamoja na Balozi wa Sweden hapa nchini Anders Sjoberg wakiminya kitufe kwa pamoja kuashiria uzinduzi wa mradi wa Ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme KV 220 kutoka Makambako hadi Songea pamoja na vituo vya kupooza umeme KV 220/33, Mradi huo mkubwa umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 215.**



**Mbunge wa Jimbo la Songea mjini na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Kima-taifa, akiwakilisha Tanzania katika mkutano wa mshikamano kuhusu suala la SAHARAWI, mkutano uliofanyika jijini Pretoria nchini Afrika ya Kusini**



**Mradi wa Kituo cha Afya Kata Ruvuma Manispaa ya Songea ambao serikali imetoa sh.milioni 400, Mradi huu unatarajia kuhudumia wakazi zaidi ya 45,000 wa Songea**



Muonekana wa mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi katika eneo la Tanga Manispaa ya Songea kwa ufadhili wa Benki ya Dunia ambao unagarimu zaidi ya shilingi bilioni 10.

Mradi huu unatekelezwa na Kam-puni ya wachina ya SIETICO kwa mkataba wa miezi 18, mradi huu ulionza Machi 2018, unatarajia kukamilika Septemba 30, 2019. Mradi umefikia asilimia 70



Makumbusho ya Taifa ya Majimaji yaliyopo Mahenge Manispaa ya Songea ni moja ya vivutio adimu vya utalii katika Mkoa wa Ruvuma. Ndani ya makumbusho haya kuna kaburi la pamoja la mashujaa 67 wa vita Majimaji ambao walinyongwa na kuzikwa pamoja mwaka 1906. Pia kuna kaburi la Jmemedari wa wangoni Songea Mbano ambaye amezikwa kiwiliwili katika kaburi la peke yake



Kamanda wa Polisi mkoani Ruvuma ACP Simon Maigwa akitoa maelezo kuhusu silaha kali ya kivita yenye uwezo wa kupiga risasi zaidi ya 700 kwa dakika moja ambayo jeshi la polisi walifanikiwa kuikamata kutoka kwa watu watano waliokuwa wanatuhumiwa kuwa ni majambazi, ambao waliuawa na Polisi wakati wanapambana na Askari kwa kurushi-ana risasi wilayani Mbinga

# Manispaa ya Songea yapata Hati Safi



**Alhaj Abdul Hassan Mshaweji**  
Mstahiki Meya Manispaa ya Songea



**MS Tina Sekambo**  
Manispaa ya Songea

HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma imepata Hati ya kuridhisha katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo Tina Sekambo amesema Halmashauri hiyo imepata Hati ya kuridhisha kuanzia mwaka wa fedha wa 2015/2016, 2016/2017 na 2017/2018.

Sekambo amebainisha mwenendo wa makusanyo kwa miaka mitatu mfululizo katika kipindi hicho cha miaka mitatu kuwa ni katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, makisio yalikuwa ni kukusanya zaidi ya bilioni 3.247 ambapo makusanyo halisi yalikuwa ni zaidi ya bilioni 1.401 sawa na asilimia 43. makusanyo halisi yalikuwa ni zaidi ya shilingi bilioni 2.697 sawa na asilimia 86.

Hata hivyo amesema hadi kufikia februari, 2019 Halmashauri hiyo, imeweza kukusanya zaidi ya bilioni 1.720 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani ukiondoa mapato ya, vituo vya Afya na Ada za Shule.

Kulingana na Sekambo, hadi kufikia Februari, 2019 Halmashauri imepokea zaidi ya shilingi bilioni 21.736 sawa na asilimia 37 ya makisio ya bajeti ya Halmashauri.

Amesema kati ya fedha hizo zaidi ya bilioni 1.843 sawa na asilimia 58 ni makusanyo ya mapato ya ndani.

Sekambo amesema zaidi ya shilingi milioni 678.72 sawa na asilimia 64 ni matumizi ya kawaida na zaidi ya shilingi bilioni 2.128 sawa na asilimia 8 ya mapokezi ya fedha za miradi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

“Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imepanga kukusanya na kutumia zaidi ya shilingi bilioni 59 kati ya fedha hizo zaidi ya bilioni 3.203 ni makadirio ya makusanyo ya mapato ya ndani, bilioni 27.751 ni Mishahara, zaidi ya bilioni 1,067 Matumizi ya kawaida (OC) na zaidi ya shilingi bilioni 27.220 ni miradi ya maendeleo. Manispaa ya Songea, inaendelea kukusanya na kudhibiti ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa LGRCIS ambapo hadi sasa kuna mashine za ukusanyaji mapato (POS) 75.

## Wanafunzi Songea kufundishwa kidijitali

SHIRIKA la Kanisa katoliki la DONBOSKO Network limetoa vishikwambi 1824 kompyuta mpakato 38 na powepoint 19 katika shule kumi za msingi katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Mhasibu wa DONBOSKO padre Celestine Kharkongor amesema vifaa hivyo vina thamani ya shilingi milioni 885 na kwamba lengo ni kuhakikisha walimu na wanafunzi wanatumia vifaa vya kielektroniki katika tendo la kujifunza na kufundisha na kuleta mapinduzi katika elimu.

Padre Celestine amesema mradi huu unafanyika katika awamu ya pili upande wa Zanzibar na wilaya Songea mkoani Ruvuma, mradi unatekelezwa katika Halmashauri za Manispaa ya Songea na Halmashauri ya wilaya ya Songea. Amesema DONBOSKO imetoa masanduku 35 yenye vishikwambi 96 kwa kilashule, power point na kompyuta

mpakato katika shule za msingi zilizopo kwenye mradi, vifaa vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.575.

Hata hivyo amesema awamu ya kwanza ya mradi huo ilianza mwaka 2017 katika shule za msingi katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Dar es Salaam, Kilimanjaro na Morogoro.

Kwa upande wake Padre Peter Mutechura ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la DONBOSKO Network Tanzania anayeshughulikia Maendeleo na elimu amesema kupitia program hii mwalimu atatumia vifaa vya kidijitali kama jukwaa la kufundishia na kuifanya wilaya ya Songea kuingia katika mfumo wa kisasa wa kufundishia. Afisa Elimu Msingi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea Zakhia Fandey amesema hiyo ni fursa nyingine katika Manispaa ya

Songea. Hata hivyo amewaagiza walimu wakuu kuhakikisha mradi unatekelezwa kulingana na malengo yaliyowekwa na vifaa hivyo visitumike katika matumizi yasiyostahili.



**Kivuko kinachounganisha Londoni Kata ya Lizaboni na Ruhuwiko Kata ya Ruhuwiko Manispaa ya Songea, kimejengwa kwa sh. milioni saba zilizotokana na mapato ya ndani hivyo kumaliza kero ya muda mrefu ya wananchi wa Songea.**



## Rais Magufuli aweka jiwe la Msingi ujenzi wa stendi ya mabasi Songea



RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Magufuli Aprili mwaka huu ameweka jiwe la msingi katika mradi wa stendi ya mabasi ya kisasa iliyopo Kata ya Tanga Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Ujenzi wa kituo kikuu cha mabasi unafanyika katika eneo lenye ukubwa wa hekari 15 umbali wa kilomita 12 toka katikati ya mji wa Songea.

Ujenzi wa kituo kikuu hicho umefikia zaidi ya asilimia 68, ulianza Machi 25, 2018 na unatarajiwa kukamilika Septemba 30, 2019. Ujenzi unafanywa na Mkandarasi CHINA SICHUAN INTERNATIONAL CORPORATION (SIETCO) na kusimamiwa na Mhandisi Mshauri BUREAU FOR INDUSTRIAL CORPORATION (BICO) ambao ni Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Tina Sekambo anasema Mradi huu unahusisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami nzito zinazolingia, kutoka na kuzunguka kituo cha mabasi zenye urefu wa kilomita mbili, Upana wa barabara zinazolingia na kutoka ni mita saba na barabara zinazozunguka kituo cha mabasi ni mita 12.

Anasema Stendi ya mabasi ya Songea pia inahusisha Ujenzi wa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 1800 la kugesha Taxi lenye uwezo wa kugesha Taksi 60 kwa wakati mmoja, Ujenzi wa Uzio mita 900. Ujenzi wa maduka 30 na Ujenzi wa ofisi za kukatia tike-ti 20.

“Maeneo mengine yanayohusika na mradi huu ni Ujenzi jengo la Utawala, Ujenzi wa vyoo, Ujenzi wa jengo litakalokuwa na Kituo cha Polisi na Ofisi za uhamiaji, Ujenzi wa kisima cha maji safi chenye urefu wa mita 75, Kuweka mfumo wa maji safi na maji taka, kuingiza umeme wa TANESCO na Kuweka Taa za sola”, anasisitiza Sekambo.

Hata hivyo anasema Mradi huu mpaka kukamilika utagharimu zaidi ya sh. bilioni 6.189.

Sekambo amebainisha kuwa Mradi huu baada ya kukamilika utaisaidia Halmashauri kuongeza bajeti ya mapato ya ndani ya mwaka 2020/2021 toka Tshs

3,749,258,100.00 mpaka Tshs 3,958,478,100.00 sawa na ongezeko la asilimia 5.29.

## TANGAZO LA LESENI ZA BIASHARA

**KWA MUJIBU WA SHERIA NAMBA 25 YA MWAKA 72 NA SHERIA YA FEDHA NAMBA 2 YA MWAKA 2014, KILA MTU AU TAASISI INAYOTOA HUDUMA AU KUUZA BIDHA ANATAKIWA KUKATA LESENI YA BIASHARA NDANI YA SIKU 21. KULINGANA NA SHERIA HIYO NI KOSA KUENDESHA BIASHARA AU KUTOA HUDUMA BILA KUWA NA LESENI YA BIASHARA. MTU YEYOTE ATAKAYEBAINIKA ANAENDESHA BIASHARA BILA KUWA NA LESENI KATIKA MANISPAA YA SONGEA ATATOZWA ADHABU ISYOPUNGUA SH. LAKI MBILI AU ISYOZIDI MILIONI MOJA. MFANYABIASHARA AU MTOA HUDUMA YEYOTE UNAKUMBUSHWA KUKATA LESENI YAKO KATIKA OFISI ZA MANISPAA YA SONGEA KUEPUKA USUMBUFU USIOKUWA WA LAZIMA.**

## Kilimo kinachangia asilimia 75 mapato ya Manispaa

Moja ya mabweni yaliyokarabatiwa katika sekondari ya Songea Girls. Serikali imetoa sh. bilioni 1.6 za kufanyia ukarabati majengo ya shule hiyo ambayo ilianzishwa mwaka 1974



SHUGHULI muhimu za kiuchumi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma ni Kilimo na biashara ambapo Kilimo huchangia asilimia 75 ya pato la Halmashauri. Mazao yanayowapatia wananchi Mapato makubwa ni Mahindi na Mpunga, aidha pato la mkazi wa Manispaa ya Songea ni **Tshs, 738,022.00** kwa mujibu wa ripoti ya GDP iliotolewa na ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2006.

Halmashauri ya Manispaa ya Songea ipo katika hatua za mwisho za kukokotoa pato la mkazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ili kujua pato la mkazi kwa mwaka.

Dira ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea ni kuwa kitovu cha uwekezaji na maendeleo ya viwanda ili kufikia maendeleo endelevu ya jamii 2025.

Halmashauri ya Manispaa ya Songea inakadiriwa kuwa na idadi ya Watu **252,150** wakiwemo Wanaume **119,182** na Wanawake **132,968** kutokana na ongezeko la asilimia **4.4** kwa mwaka,

## Wafanyabiashara wasalimisha tani 1.7 za mifuko plastiki

MANISPAA ya Songea mkoani Ruvuma imeanza kutekeleza Mpango kabambe wa kutoa elimu kwa wafanyabiashara ili kusalimisha mifuko ya plastiki ambayo imepigwa marufuku kuanzia Juni Mosi mwaka huu. Katika siku ya kwanza ya kutekeleza mpango huu wafanyabiashara wanne katika Manispaa ya Songea wamesalimisha KG 1778 sawa na zaidi ya tani 1.7 za mifuko ya plastiki ambapo utekelezaji wa kuhakikisha mifuko yote ya rambo katika Manispaa ya Songea inatoweka utakuwa ni endelevu ili mji wa Songea uwe safi wakati wote.



Pichani Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Songea ikiongozwa na Katibu wa CCM Wilaya ya Songea Juma Ally Mpeli katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2015 ndani ya Manispaa ya Songea. Hapa ni kiwanda cha Mohamed Enterprises chenye uwezo wa kusaga unga tani 100 kwa siku.



Serikali ya Awamu ya Tano imeleta sh. bilioni 37 kufanyia ukarabati wa uwanja wa ndege wa Songea ambao ulijengwa kati ya mwaka 1974 hadi 1980

Baraza la Madiwani la Manispaa ya Songea



IDARA ya Makumbusho ya Taifa kwa kushirikiana na ofisi ya Maliasili na utalii Mkoa wa Ruvuma imeleta vipande viwili vya magogo yanayogeuka mawe kutoka pori la Selous na kuviweka katika Kituo cha Habari za Utalii cha Mkoa wa Ruvuma kili-chopo ofisi za maliasili Mahenge mjini Songea.

.Mara baada ya kufunguliwa rasmi Kituo cha Habari za Utalii cha Mkoa wa Ruvuma vipande vya magogo yanayogeuka mawe ni miongoni mwa vivutio adimu vya utalii ambavyo vimewekwa katika Kituo hicho.

## Manispaa ya Songea yapima viwanja zaidi ya 35,000

.HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma ina jumla ya viwanja 35,500 vilivyopimwa katika maeneo mbalimbali ya Manispaa hiyo. Mkurugenzi wa Manispaa hiyo Tina Sekambo amesema Kati ya hivyo viwanja 18,489 ramani zake zimesajiliwa na kwamba maeneo ambayo ramani zake hazijasajiliwa yameundiwa kamati Kwa kuwashirikisha Wananchi ili kukamilisha Upimaji kwa njia ya Upimaji shirikishi.

“Halmashauri imetekeleza agizo la serikali kwa kuhakikisha maeneo yote ya umma yanapimwa na kuandaliwa hati. Maeneo hayo yanajumuisha vituo vya afya, Maneo ya shule ZA Msingi na Sekondari, Zahanati pamoja na Ofisi za Umma”, alisema Hata hivyo Sekambo amesema, hadi sasa jumla ya maeneo 170 yamepimwa na mengine yamepimwa kwa hatua ya awali (Demarcation) na mchakato wa

Mkurugenzi wa Makumbusho ya Taifa ya Majimaji Balthazar Nyamusya anatoa rai kwa watazania kutembelea katika Kituo hicho na Makumbusho ya Taifa ya Majimaji ili kujifunza rasilimali muhimu ya Taifa. Miti inayogeuka mawe inatoka katika Pori la akiba la Selous lilianzishwa mwaka 1896 na wajerumani likiwa ni pori la kwanza kutengwa kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori katika Bara la Afrika na la pili duniani kwa ukubwa baada ya hifadhi ya pori la Marekani ambalo linaitwa Yellowstone. Hata hivyo utafiti wa kimataifa umebaini miti inayogeuka mawe iliyopo pori la Selous Tanzania inapatikana pia kaskazini mwa Afrika katika nchi za Misri, Libya na Algeria, pia miti hiyo inapatikana katika nchi ya Ugiriki na Marekani.

kukamilisha upimaji huo unafanyika na ramani hizo zinasajiliwa.

Kulingana na Mkurugenzi huyo, Halmashauri ya Manispaa ya Songea, imeandaa Mpango kabambe (MasterPlan) ambao umeidhinishwa na Wizarra na utatumika katika kipindi cha miaka 20 (2017-2037) kama dira ya maendeleo ya Mji wa Songea.

## **TANGAZO KUPATA LESENI YA BIASHARA, KWA NJIA RAHISI, TAFADHALI TEMBELEA KITENGO CHA BIASHARA KATIKA MANISPAA YA SONGEA CHUMBA**

**NO .10**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma imetoa mkopo wa zaidi ya milioni 61 katika vikundi 48 vya wajasiriamali wadogo.

Akisoma taarifa ya utoaji mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na makundi maalum kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Naftali Saiyoloi amesema fedha hizo zimetokana na mapato ya ndani ya asilimia kumi. Amesema fedha zinazokopeshwa ni mapato ya ndani ya shilingi milioni 40 na fedha za marejesho ya mikopo ambazo ni shilingi milioni 21 na kwamba mikopo inatolewa ili kukamilisha utoaji wa mikopo ya robo ya mwaka wa fedha wa 2018/2019.

“Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 jumla ya vikundi vya wanawake 127 vimekopeshwa shilingi milioni 33.9 hivyo kufanya jumla ya fedha zilizokopeshwa kufikia milioni 196”, alisisitiza Saiyoloi. Mgeni rasmi katika hafla hiyo Mkuu wa Wilaya ya Songea Polelet Mgema amesema serikali imekwishaagiza kuanzia mwaka wa fedha wa 2018/2019 hakutakuwepo tena na tozo ya riba ya asilimia 10 kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma. “Fedha hizi mnaazimwa mkazifanyie kazi na baadaye mzirejeshe, fedha hizi ni za kwenu wanawake, vijana na makundi maalum waliopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea, tunapeana kwa zamu”, alisisitiza Hata hivyo Mkuu wa Wilaya ameagiza wale wote waliopewa mikopo kuirejesha kwa wakati ili zitumike kuwakopesha wajasiriamali wadogo wengine na kufanya biashara yenye tija kwa kuwa na mkopo mkubwa.

Halmashauri ya Manispaa ya Songea katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2018/2019 imeweza kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na makundi maalum kwa asilimia 91.8

Jumla ya fedha za marejesho ni milioni 124.8 na kufanya jumla kuu kuwa sh. milioni 285.5

## Manispaa yapokea zaidi ya bilioni 1.229 za Elimu bila Malipo

ZAIDI ya sh.bilioni 1.229 zimepokelewa na Halmashauri ya Manispaa ya Songea katika kipindi cha mwaka 2017/2018 kupitia Mpango wa Elimu bila malipo kwa ajili ya shule za msingi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Tina Sekambo amesema katika kipindi cha Januari hadi Machi 2019 „Halmashauri imepokea zaidi zaidi ya shilingi milioni **424.324 ambapo** wa Capitation ni **zaidi ya 189.578**, Chakula ni **na zaidi ya milioni 71 zilitolewa kwa** Walimu wakuu n fedha za madaraka. Ambapo sh.**121,600,000.00** za Waratibu wa Elimu kata kwa ajili ya Fedha za madaraka) ni **Tshs.42,324,000.00**

Amesema Upatikanaji wa fedha hizi umeboresha miundombinu ya madarasa, vyoo, samani, upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia mashuleni na hivyo kufanya kazi ya ufundishaji kuwa rahisi kwa Walimu sawa na asilimia 100 ya utekelezaji wa fedha zilizopokelewa za Elimu Bila mali

Amesema kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imepokea fedha ya miradi wa Lipa kulingana na matokeo (P4R) zaidi ya shilingi milioni **608.362**.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Tina Sekambo amesema Kati ya fedha hizo zaidi ya milioni **445.662** zilipelekwa Idara ya Elimu msingi.

## Songea kuzalisha miche ya kahawa 143,384

HALMASHAURI ya Manispaa ya Songea ina mpango wa kuzalisha miche ya Kahawa 143,384 katika vitalu 6 kwa msimu wa 2018/2019. Miche 121,784 inatajiwa kupandwa katika ukubwa Hekta 72.94 na wakulima 290 watanufaika.

Msimu wa 2016/2017 wakulima walitumia pembejeo kiasi cha tani 19,450 za mbolea, kati ya hizo mbolea tani 173.8 zilikuwa ni za ruzuku ya Serikali. Pembejeo hizo zilitumika Katika mazao ya mahindi, kahawa na mpunga. Halmashauri ina maduka ya pembejeo za kilimo 45 na makampuni 6 ya pembejeo.

Katika msimu wa Kilimo wa mwaka 2017/2018 mbolea ya Kupandia na kukuzia zipo katika mfumo wa manunuzi wa pamoja (BPS – Bulk Procurement Supply), ambapo serikali imetoa bei elekezi kwa mbolea hizo. Mbolea ya kupandia (DAP) Tsh. 54,236/=

## Migogoro ya ardhi 39 yatatuliwa Songea

MIGOGORO ya Ardhi ni moja ya matatizo yanayoikabili Manispaa ya Songea.

Katika kipindi cha Mwaka 2018/2019 Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea Migogoro **48**, ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ikishirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na Ofisi ya Kamishina Masaidizi wa Kanda ya kusini Mtwara imefanikiwa kutatua migogoro **39**.

Migogoro **9** iliyobaki ipo katika hatua za utatuzi na mingine ipo Mahakamani. Vyanzo vya migogoro hiyo ni fidia ya Ardhi iliyotwaliwa kwa shughuli za Umma na wenyeji wa kuvamia na kuuza maeneo yaliyokwishapimwa.

Migogoro **9** iliyobaki miwili ni migogoro ya fidia ya EPZA na SOWASA ambapo Uthamini wa fidia eneo la EPZA Mwengemshindo ulifanyika mwaka **2008** ambapo Wananchi waliofanyiwa uthamini ni **2,150** waliokuwa wanastahili kulipwa Jumla ya **Tshs. 2,805,027,258.00** Uthamini huo wa fidia ulijumuisha ardhi, mazao na nyumba na eneo lililotwaliwa lina ukubwa ekari **5000**.



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Songea John Sokwe akizungumiza serikali kutoa zaidi ya sh.milioni 952 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa majengo na miundombinu ya shule hiyo kongwe ambayo ilianzishwa mwaka 1950 .

**JARIDA HILI LIMETOLEWA NA  
HALMASHAURI YA MANISPAA  
YA SONGEA**

**BODI YA UHARIRI**

**1.TINA SEKAMBO  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
YA SONGEA**

**2.ALBANO MIDELO  
AFISA HABARI MANISPAA YA  
SONGEA**

**3.UPENDO BONAMALI  
AFISA TAKWIMU MANISPAA  
YA SONGEA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA**  
Anuani ya Posta: P O BOX 14,  
SONGEA  
Simu ya Mezani: 025 2602970  
Simu ya Kiganjani:  
Baruapepe [info@songeamc.go.tz](mailto:info@songeamc.go.tz)  
Tovuti: [songeamc.go.tz](http://songeamc.go.tz)

## TANGAZO



**MKURUGENZI WA  
HALMASHAURI YA  
MANISPAA YA  
SONGEA ANAWATAN-  
GAZIA WANANCHI  
WOTE WA MANISPAA  
YA SONGEA KUJIT-  
OKEZA KWENYE  
USAFI WA MAZINGIRA**

**KATIKA MITAA NA MAKAZI YAO JUMAMO-  
SI YA KILA MWISHO WA MWEZI .  
KUFANYA USAFI JUMAMOSI YA MWISHO  
WA MWEZI NI TAKWA LA  
KISHERIA,MNAOMBWA WOTE KUSHIRIKI**

[Songeamc.go.tz](http://Songeamc.go.tz)

## TANGAZO

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA  
SONGEA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA  
ANAUZA VIWANJA VILIVYOPIMWA KATIKA ENEO LA  
LILAMBO NA NAMANDITI KWA MATUMIZI YA MAKAZI.**

**BEI YA VIWANJA HIVYO NI SHILINGI 2000 KWA KILA  
MITA MOJA YA MRABA.VIWANJA HIVYO VIPO PEM-  
BEZONI MWA BARABARA YA SONGEA-  
MBINGA,UMBALI WA KILOMETA 12 KUTOKA KATIKATI  
YA MJI.**

**MIUNDOMBINU WEZESHI YAANI MAJI,BARABARA NA  
UMEME ZIPO KWENYE ENEO LA MRADLAIDHA  
BARABARA ZOTE ZA NDANI YA MIRADI ZITACHONG-  
WA NA ZITAPITIKA WAKATI WOTE.**

**FOMU ZA MAOMBI ZINAPATIKANA KATIKA OFISI YA  
IDARA YA ARDHI NA MIPANGO MIJI YA HALMASHAURI  
YA MANISPAA YA SONGEA KUANZIA SAA 3.00 ASUBUHI  
HADI SAA 9.00 ALASIRI KUANZIA SIKU YA JUMATATU  
HADI IJUMAA,BEI YA FOMU NI SHILINGI 20,000 KWA  
KILA FOMU MOJA NA GHARAMA HIYO HAITARUDISH-  
WA.**

**TANGAZO LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA  
MANISPAA YA SONGEA**

## Gombeeni uongozi serikali za mitaa



NAIBU Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea Judith Mbogoro ametoa rai kwa wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea uongozi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika baadaye mwaka huu.Mbogoro alikuwa anazungumza katika wiki ya maadhimisho ya siku ya wanawake duniani ambayo kilele chake kilikuwa ni Machi 8 ambapo katika Manispaa ya Songea uzinduzi ulifanyika kwenye bustani ya Manispaa ya Songea na kilele chake kilifanyika Namanditi Kata ya Ruhuwiko Manispaa ya Songea. Ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Songea Jaji Sekela Moshi.

# Taarifa ya TAKUKURU Ruvuma kuanzia Aprili hadi Juni 2019



Yustina Chagaka Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma

Kuhusu mabaraza ya ardhi Chagaka amesema mabaraza ya ardhi ya Kata yanafanya kazi za kisheria, wakati hawana elimu ya sheria jambo linalosababisha kuongezeka kwa vitendo vya rushwa katika Idara ya ardhi wakati wa kutatua migogoro baina ya mlalamikaji na mlalamikiwa.

“Katika kipindi cha miezi mitatu TAKUKURU mkoani Ruvuma imepokea taarifa za malalamiko ya rushwa 63 toka vyanzo mbalimbali ambapo kati ya malalamiko hayo idara ya ardhi inaongoza kwa kulalamikiwa kwa malalamiko 17”, alisema.

Ameitaja Idara inayofuatia kwa kulalamikiwa kuwa ni idara ya elimu yenye malalamiko 10 na ya mwisho kulalamikiwa ni taasisi za kifedha zenye malalamiko mawili.

Aidha TAKUKURU Ruvuma imefanya ufutiliaji wa zaidi ya shilingi bilioni 14 ambazo zimetolewa na serikali kwa ujenzi wa miradi ya miundo mbinu ya ujenzi, maji, afya, elimu na barabara nakubaini dosari ndogondogo ambazo zimeshatolewa ushauri wa wanamna ya kurekebisha dosari hizo.

Akizungumzia kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika nchini baadaye mwaka huu, Chagaka amewataka wagombea na wapiga kura kujiepusha na vitendo vya rushwa ambavyo vitawasababishia matatizo ya kuchukuliwa hatua za kisheria kulingana na sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa namba 11 ya mwaka 2007 ya kuongoza vita dhidi ya rushwa na uufisadi nchini.

TAKUKURU Mkoa wa Ruvuma imeendelea kutekeleza matakwa ya Sheria inayoongoza majukumu matatu ambayo ni kuzuia rushwa, kuelimisha umma na kuchunguza tuhuma za rushwa na kushitaki watuhumiwa.

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU mkoani Ruvuma imefanya uchambuzi wa mifumo mitatu ili kubaini mianya ya rushwa katika sekta ya Elimu katika usimamizi wa mitihani ya kitaifa.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Ruvuma Yustina Chagaka akitoa taarifa ya utendajikazi wa TAKUKURU katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Aprili hadi Juni 2019 kwa wanahabari mjini Songea, amesema mianya hiyo imechunguzwa katika Halmashauri za Manispaa ya Songea, Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Madaba.

Amesema katika kipindi hicho TAKUKURU ilifanya ufutiliaji wa utekelezaji wa maazimio ya warsha ya wadau kuhusu mfumo wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ujazaji fomu za afya kwa wanafunzi wanaoanza masomo ya sekondari katika Halmashauri za Mji Mbinga na kuokoa kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 22.

Kamanda wa TAKUKURU mkoani Ruvuma Christina Chagaga ametoa wito kwa Halmashauri kutoa elimu ya sheria kwa mabaraza ya ardhi ya Kata.

# MICHEZO

Songea ilivyofanikiwa kuwa mshindi wa jumla katika UMISETA 2019



Mwaka 2019 umekuwa ni mwaka wa mafanikio makubwa katika michezo kwa Halmashauri ya Manispaa ya Songea na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla wake. Katika Mashindano ya UMISETA kitaifa yaliofanyika mkoani Mtwara. Mkoa wa Ruvuma umekuwa mshindi wa jumla katika soka wawulana,, Pia Mkoa wa Ruvuma umekuwa mshindi wa kwanza katika mchezo wa mpira wa meza na mshindi wa kwanza katika mchezo wa kikapu wawulana.

Manispaa ya Songea katika mashindano wa UMISETA ngazi ya Mkoa wa Ruvuma mwaka 2019, imekuwa ni mshindi wa jumla katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma.